TAARIFA YA MATOKEO YA MITIHANI YA TAIFA YA MWAKA 2020

UTANGULIZI

Ndugu Wanafunzi, Walimu, Wazazi, Wanahabari na Wananchi kwa ujumla Assalaamu alaykum, leo tumekutana hapa kwa ajili ya kutoa Taarifa ya Matokeo ya Mitihani ya Taifa ya mwaka 2020 kama ilivyo kawaida yetu kila mwaka.

Mitihani ya Taifa ya Darasa la Nne, Darasa la Sita na Kidato cha Pili hufanywa kwa lengo la kupima na hatimaye kujua kiasi cha Maarifa, Ujuzi na Muelekeo wa Wanafunzi walioupata katika kipidi chote cha kujifunza.

Matokeo haya yatawasaidia Wanafunzi katika kuongeza bidii na ari ya kujifunza katika madarasa yanayofuata. Aidha mrejesho wa matokeo ya mitihani hii utawasaidia Walimu kuweza kuimarisha mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya kukuza uelewa wa Wanafunzi na hatimaye kuinua kiwango cha ufaulu na ubora wa elimu nchini.

Matokeo ya Mitihani hii pia yatatumika katika kuwapanga wanafunzi katika ngazi ya juu kutoka ngazi aliyopo sasa.

UANDIKISHWAJI NA MAHUDHURIO

DARASA LA NNE

Jumla ya watahiniwa **50,952** waliandikishwa kufanya mtihani huo katika Skuli **441** kati ya hizo **283** ni za Serikali na **156** ni za Binafsi, kati yawanafunzi walioandikishwa Wanawake ni **24,872** sawa na asilimia **48.8** na Wanaume

ni **26,08** sawa na asilimia **51.2.** Idadi hii imepungua kwa watahiniwa **4,679** sawa na asilimia **9.2** ikilinganishwa na watahiniwa **55,631** walioandikishwa kwa mwaka 2019.

Watahiniwa **48,246** sawa na asilimia **94.7** walifanya mtihani huo ambapo wanawake ni **24,119** sawa na asilimia **49.99** na wanaume ni **24,127** sawa na asilimia **50.01.** Aidha, jumla ya watahiniwa **2,706** sawa na asilimia **5.31** hawakufanya mtihani huo kutokana na utoro na ugonjwa.

DARASA LA SITA

Uandikishwaji wa watahiniwa wa Mtihani wa Taifa wa Darasa la Sita ulifanyika katika Skuli **397,** kati ya Skuli hizo, Skuli **275** ni za Serikali na **122** ni za Binafsi. Kuna ongezeko la Skuli **17** sawa na asilimia **1.4** ikilinganishwa na Skuli zilizoandikishwa mwaka 2019.

Watahiniwa **34,218** waliandikishwa kufanya mtihani huo kati yao Wanawake ni **17,835** na asilimia **52.12** na Wanaume ni **16,383** sawa na asilimia **47.88** Idadi hii imeongezeka kwa watahiniwa **1,910** sawa na asilimia **5.5** ilinganishwa na watahiniwa **32,308** walioandikishwa mwaka 2019. Watahiniwa **33,010** walifanya mtihani huo sawa na asilimia **96.46** ambapo wanawake ni **17,482** sawa na asilimia **51.09** na wanaume **15,528** sawa na asilimia **45.37.** Aidha watahiniwa **1,208** sawa na asilimia **3.53** hawakufanya Mtihani huo kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo utoro na ugonjwa.

KIDATO CHA PILI

Uandikishwaji wa watahiniwa wa Kidato cha Pili ulifanyika katika Skuli **271** kati ya skuli hizo, Skuli **204** ni za Serikali na **67** ni za Skuli Binafsi. Kuna upungufu wa Skuli **06** ikilinganishwa na Skuli za Kidato cha Pili za mwaka 2019.

Jumla ya watahiniwa **33,792** walioandikishwa kufanya mtihani huo kati yao wanawake ni **18,347** sawa na asilimia **54.29** na wanaume ni **15,445** sawa na asilimia **45.71.** Idadi hii ni pungufu kwa watahiniwa **681** sawa na asilimia **1.98.**

KESI ZA UDANGANYIFU

Katika Mitihani ya Mwaka 2020 hakukuwa na kesi yoyote ya udanganyifu kwa Darasa la Nne na Sita. Isipokuwa Kwa Kidato cha Pili, kesi moja ya Udanganyifu imebainika kwa Mtahiniwa mwenye nambari ya Mtihani **ZS.108/012/2020** wa Kituo cha Mtihani cha Skuli ya Cheju ambaye amepatikana na karatasi zenye maandishi (notes) ya somo la Historia ndani ya chumba cha mtihani akiwa anafanya mtihani. Kwa hivyo kwa mujibu wa kanuni za Mitihani za Baraza la Mitihani la Zanzibar Kifungu cha 58(1) mtahiniwa huyo amefutiwa matokeo yake ya mtihani.

MATOKEO KWA DARASA LA NNE

Ufaulu unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa **39,273** sawa na asilimia **81.4** wamefaulu wakiwemo wanawake **21,162** sawa na asilimia **43.86** na

wanaume **18,111** sawa na asilimia **37.54** Wanafunzi **8,973** sawa na asilimia **18.6** hawakufaulu.

Ufaulu huu umepanda kwa asilimia **1.1** ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia **80.5** wa mwaka 2019. Matokeo yanaonesha kuwa ufaulu katika daraja A,B, na C umepanda kwa kuwa na asilimia **40.8** ikilinganishwa na asilimia **39.9** ya mwaka 2019.

UFAULU KIWILAYA

Katika Mtihani huu Wilaya ya Mjini inaongoza kwa Ufaulu wa Jumla kwa kuwa na asilimia **91.26** ikifuatiwa na Wilaya Chake Chake yenye asilimia **87.35.** Aidha Wilaya ya Mkoani ni ya mwisho kwa kuwa asilimia ya ufaulu ya **67.42.**

MATOKEO KWA DARASA LA SITA

Ufaulu unaonesha kuwa jumla ya watahiniwa **32,462** sawa na asilimia **98.34** kati ya **33,010** waliofanya mtihani huu wamefaulu kwa madaraja ya **A, B, C** na **D** na watahiniwa **548** sawa na asilimia **1.66** hawakufaulu.
Ufaulu huo umepanda kwa asilimia **0.84** ukilinganishwa na ufaulu wa asilimia **97.5** wa mwaka 2019.

Idadi ya watahiniwa waliofaulu ambao wenye sifa ya kuendelea na masomo ya Kidato cha kwanza katika madarasa ya Vipawa (**209**), Michepuo (**1,612**) na Sekondari za kawaida (**30,641**) imeongezeka kwa mwaka 2020. Aidha Ubora wa ufaulu unaonesha kuwa idadi ya watahiniwa waliofaulu kwa daraja **A, B** na **C** umepanda kwa kuwa na asilimia **47.04** ikilinganishwa na asilimia **41.3** ya mwaka 2019.

UFAULU KIWILAYA

Wilaya zote zimefanya vizuri ambapo Wilaya ya Micheweni ikiongoza kwa Ufaulu wa Jumla wa asilimia **99.78** ikifuatiwa na Wilaya Chake Chake yenye asilimia **99.05.**

MATOKEO KWA KIDATO CHA PILI

Jumla ya watahiniwa **25,593** sawa na asilimia **78.67** kati ya **32,279** waliofanya mtihani huu wamefaulu kwa madaraja ya **A, B^+,B, C** na **D** na watahiniwa **6,886** sawa na asilimia **21.33** hawakufaulu.

Ufaulu huu umepanda kwa asilimia **3.5** ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia **76.8** wa mwaka 2019, ambapo idadi ya watahiniwa waliopata daraja **A,B^+,B na C** umeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019.

UFAULU KIWILAYA

Wilaya zote zimefanya vizuri ambapo Wilaya ya Chake Chake inaongoza kwakupata ufaulu wa Jumla wa asilimia **86.89** na Wilaya ya Kusini ni ya mwisho yenye wa jumla wa asilimia **61.32.**

WANAFUNZI WALIOFANYA VIZURI ZAIDI KITAIFA

Matokeo yanaonesha kuwa wanafunzi kumi waliofanya vizuri zaidi Kitaifa kwa madarasa yote ya mitihani wametokea Skuli za mijini.

WATAHINIWA KUMI BORA KITAIFA KWA DARASA LA NNE

Mwanafunzi **Veronica Paul Mwendesha** kutoka Skuli ya Upendo anaongoza kwa Darasa la Nne.

NA.	NAMBA YA MTAHINIWA	JINA LA MTAHINIWA	JINSI	JINA LA SKULI	WILAYA	WASTANI
1.	ZP.435/013/20	VERONICA PAUL MWENDESHA	MKE	UPENDO PRIMARY	MAGHARIBI A	90.5
2.	ZP.180/227/20	ZAHDI SAID OMAR	MME	MITIULAYA	WETE	90.25
3.	ZP.435/003/20	CHRISTINA KURWA PETRO	MKE	UPENDO PRIMARY	MAGHARIBI A	89.5
4.	ZP.435/023/20	SLEYUM RASHID SAID	MME	UPENDO PRIMARY	MAGHARIBI A	87.75
5.	ZP.402/009/20	HAWA AMOUR SALUM	MKE	GREAT VISION	MAGHARIBI B	87
6.	ZP.448/014/20	UMIHILDA USSI MOHAMED	MKE	AL-KHAIRAT MADRASAT ISLAMIYA	MAGHARIBI A	86.5
7.	ZP.402/043/20	LEWIS MATEO KANUTI	MME	GREAT VISION	MAGHARIBI A	86.25
8.	ZP.356/007/20	GHANIA TWAHA MGENI	MKE	MADRASATUL-AHBAAB	MAGHARIBI B	85.75
9.	ZP.180/071/20	RAHMA MOH'D ABRAHMAN	MKE	MITIULAYA	WETE	85.5
10.	ZP.453/009/20	ZUHURA JUMA AHMED	MKE	NEW GOLDEN ACADEMY	MAGHARIBI A	85.5

SKULI KUMI ZILIZOFANYA VIZURI KITAIFA KWA DARASA LA NNE
SKULI ZENYE WATAHINIWA 45 NA ZAIDI

Skuli za binafsi zinaonekana kufanya vizuri ikilinganishwa na skuli za Serikali.

JINA LA SKULI	WILAYA	IDADI YA WATAHINIWA	WASTANI
GREAT VISION	MAGHARIBI A	53	68.99
MADRASATUL-AHBAAB	MAGHARIBI B	47	63.48
ALI KHAMIS CAMP	CHAKECHAKE	83	59.68
FRANCIS MARIA	MAGHARIBI B	86	56.33
BRIGHT FUTURE ACADEMY (B)	MAGHARIBI B	68	52.22
GLORIOUS ACADEMY (B)	MJINI	363	51.67
BRILLIANT ACADEMY (B)	MAGHARIBI A	132	51.09
LAUREAT INTERNATIONAL	MAGHARIBI B	119	50.56
KARIBU SCHOOL	MAGHARIBI A	47	49.59
SOS HERMAN	MAGHARIBI B	75	48.65

SKULI KUMI ZILIZOFANYA VIZURI KITAIFA DARASA LA NNE

SKULI ZENYE WATAHINIWA CHINI YA 45

Skuli za binafsi zinaonekana kufanya vizuri ikilinganishwa na skuli za Serikali

JINA LA SKULI	WILAYA	IDADI YA WANAFUNZI	WASTANI
UPENDO PRIMARY	MAGHARIBI A	25	68.78
EDEN INTERNATINAL SCHOOL	MAGHARIBI B	13	68.04
AL-KHAYRAT MADRASAT ISLAMIYA	MAGHARIBI A	23	65.92
FEZA SCHOOL	MAGHARIBI B	36	62.86
NEW GOLDEN ACADEMY	MAGHARIBI A	19	61.39
COSMOS PRE ,PRIMARY SCHOOL	MAGHARIBI B	15	59.03
WINNERS SCHOOL ACADEMY	KATI	18	53.18
BRITISH SCHOOL	MAGHARIBI B	14	52
INTELLIGENT KIDS ACADEMY	MJINI	29	51.11
EDUCATION PLUS ACADEMY	MAGHARIBI A	11	50.89

WATAHINIWA KUMI BORA KITAIFA DARASA LA SITA

Mwanafunzi **Khalil Shaido Abdulrazak** kutoka Skuli ya High-View International anaongoza kwaDarasa la Sita.

Na.	NAMBA YA MTAHINIWA	JINA LA MTAHINIWA	JINSI	WILAYA	JINA LA SKULI	WASTANI	
1.	ZP.311/043/20	KHALIL SHAIDO ABDULRAZAK	MME	MAGHARIBI B	HIGH-VIEW INTERNATIONAL	84.96	1
2.	ZP.045/119/2020	MOHAMED SHAMTE SALEH	MME	MAGHARIBI B	M/KWEREKWE 'F'	84.66	2
3.	ZP.180/011/2020	FATMA HAFIDH MBAROUK	MKE	WETE	MITIULAYA	84.34	3
4.	ZP.305/007/2020	SUMAYYA KHAMIS HUSSEIN	MKE	MAGHARIBI B	YURIZ ACADEMY	83.86	4
5.	ZP.203/040/2020	SHARIFA HAMAD KHAMIS	MKE	MICHEWENI	KINOWE	83.82	5
6.	ZP.005/042/2020	FIRDAUSI ALI AYOUB	MKE	MJINI	KISIWANDUI	83.76	6
7.	ZP.040/084/2020	RAHMA SAID HAMADI	MKE	MAGHARIBI B	M/KWEREKWE 'D'	82.6	7
8..	ZP.005/199/2020	ARQAM SAID JUMA	MME	MJINI	KISIWANDUI	82.26	8
9.	ZP.356/014/2020	ABUUBAKAR SAID SEIF	MME	MAGHARIBI B	MADRASATUL-AHBAAB	81.78	9
10.	ZP.204/009/2020	FATMA AMOUR MBAROUK	MKE	MICHEWENI	SIZINI	81.68	10

SKULI KUMI ZILIZOFANYA VIZURI KITAIFA DARASA LA SITA

SKULI ZENYE WATAHINIWA 45 NA ZAIDI

Skuli za binafsi zinaonekana kufanya vizuri ikilinganishwa na skuli za Serikali.

JINA LA SKULI	WILAYA	IDADI YA WATAHINIWA	WASTANI
GREAT VISION SCHOOL	MAGHARIBI A	45	67.39
BRILLIANT ACADEMY	MAGHARIBI A	47	63.26
S.O.S HERMANN	MAGHARIBI B	90	58.20
FEZA	MAGHARIBI B	49	58.18
GLORIOUS ACADEMY	MJINI	274	56.17
TRIFONIA ACADEMY	MAGHARIBI B	67	54.76
LAUREATE INTERNATIONAL	MAGHARIBI B	119	53.9
HIGH-VIEW INTERNATIONAL	MAGHARIBI B	54	53.4
FRANCIS MARIA	MAGHARIBI B	85	51.93
AL-HARAMYN INTERNATIONAL	MAGHARIBI B	96	51.21

SKULI ZILIZOFANYA VIZURI KITAIFA DARASA LA SITA

SKULI ZENYE WATAHINIWA CHINI YA 45

JINA LA SKULI	WILAYA	IDADI YA WATAHINIWA	WASTANI
MADRASATUL-AHBAAB	MAGHARIBI B	28	71.39
EVERGREEN SCHOOL	MAGHARIBI B	15	61.46
THE PALM ACADEMY	KATI	17	60.05
DALUAA ISLAMIC	CHAKE CHAKE	12	58.99
EDEN INT SCHOOL	MAGHARIBI B	12	58.76
JABAL KHIRAA INTERGRATED	MAGHARIBI B	09	58.62
THE LION KING	MAGHARIBI B	15	57.98
SUFA	MAGHARIBI B	29	57.89
HERRN HUTER ACADEMY	MAGHARIBI A	10	57.36
AL-MARFAA ISLAMIC SCHOOL	MAGHARIBI B	28	56.68

WATAHINIWA KUMI BORA KITAIFA KIDATO CHA PILI

Mwanafunzi **Abdul-Latif Salum Sharif** kutoka Skuli ya Fidel-Castro anaongoza kwaKidato cha Pili.

NAMBA YA MTAHINIWA	JINA LA MTAHINIWA	JINSI	WILAYA	JINA LA SKULI	WASTANI	NATIJA
ZS.189/032/20	ABDUL-LATIF SALUM SHARIF	M	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	82.32	1
ZS.189/046/20	SULEIMAN HAFIDH MBAROUK	M	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	82.18	2
ZS.189/031/20	ABDILLAH MOH'D KASSIM	M	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	81.91	3
ZS.189/039/20	LUKMAN ALI FAKI	M	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	81.54	4
ZS.233/044/20	ZIHRA ABDULHALEEM HAMDOUN	F	MAGHARIBI B	LAUREATE INT	81.03	5
ZS.232/017/20	SHEIKHA SALEH AL-SHEIKH	F	MAGHARIBI B	FEZA	78.92	6
ZS.189/011/20	JAMILA MOH'D SALEH	F	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	78.76	7
ZS.189/034/20	AYOUB ALI MOHAMMED	M	CHAKE CHAKE	FIDELCASTRO	78.62	8
zs.286/038/20	MAHMOUD HABIB ABEID	M	MAGHARIBI A	BRILLIANT ACADEMY	78.15	9
ZS.232/028/20	KASSIM SHAABAN SALIM	M	MAGHARIBI B	FEZA	78	10

SKULI KUMI ZILIZOFANYA VIZURI KITAIFA KIDATO CHA PILI

SKULI ZENYE WATAHINIWA 45 NA ZAIDI

Skuli za Serikali zinaonekana kufanya vizuri ikilinganishwa na skuli za Binafsi.

JINA LA SKULI	WILAYA	IDADI YA WATAHINIWA	WASTANI
FIDELCASTRO	CHAKE CHAKE	49	71.21
LUMUMBA	MJINI	78	65.61
MOH'D JUMA PINDUA	MKOANI	66	60.53
MADUNGU 'B'	CHAKE CHAKE	54	59.25
MIKINDANI DOLE	MAGHARIBI A	102	56.83
ZANZIBAR COMMERCIAL	MAGHARIBI B	127	55.56
GLORIOUS ACADEMY	MJINI	130	54.49
TUMEKUJA	MJINI	131	51.23
KIEMBE SAMAKI A	MAGHARIBI B	98	50.84
BEN-BELLA	MJINI	158	49.48

SKULI ZILIZOFANYA VIZURI KITAIFA KIDATO CHA PILI

SKULI ZENYE WATAHINIWA CHINI YA 45

JINA LA SKULI	WILAYA	IDADI YA WANAFUNZI	WASTANI
FEZA	MAGHARIBI B	36	60.22
KENGEJA UFUNDI	MKOANI	35	55.69
BRILLIANT ACADEMY	MAGHARIBI A	43	54.91
CCK KIUYU	MICHEWENI	43	54.25
LAUREATE INT. PEMBA	CHAKE CHAKE	12	52.08
UTAANI 'B'	WETE	38	50.88
ASFAT ISLAMIC SCHOOL	MAGHARIBI B	14	49.69
AL-MARFAA ISLAMIC SCHOOL	MAGHARIBI B	20	43.64
STEP-UP ACADEMY	MAGHARIBI B	26	43.48
MWERA SUPER	MAGHARIBI A	27	43

PONGEZI ZA WIZARA

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa dhati kabisa inawapongeza wanafunzi wote waliofaulu katika mitihani yao kwa kuweza kuendelea na masomo katika madarasa yanayofuata na wanaombwa kuongeza bidii ili waweze kukuza uwezo wao wa kitaaluma kwa ajili ya kupata ufaulu mzuri zaidi katika mitihani ijayo. Aidha Wizara inatoa pongezi kwa Walimu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwapatia wanafunzi taaluma na maadili mema mambo ambayo yatawasaidia wakati wa sasa na baadae.

Pia Wizara inaendelea kuwashukuru Wazazi na walezi wa wanafunzi kwa kuwasimamia, kuwalea, kuwaongoza na kuwapatia watoto wao huduma za lazima ili waweze kumudu masomo yao.

Aidha Wizara inatoa shukurani kwa wale wote walioshiriki katika kufanikisha ufanyaji wa mitihani hii katika hatua zake zote.

Kuangalia matokeo.

Ndugu wanafunzi, Walimu na Wananchi kwa ujumla, Wizara inapenda kuwaarifu kwamba matokeo ya mitihani hii yanaonekana katika tovuti zifuatazo.

www.moez.go.tz na

www.bmz.go.tz

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

Simai Mohammed Said (MBM),
Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
Zanzibar.